# TERM 2 2022 OPENER EXAM FORM 3
# KISWAHILI
# LUGHA
# MAAKIZO:

**1. UFAHAMU**
**Soma makala yafuatayo kisha ujibu maswali. (alama 15)**

Mojawapo kati ya misingi na nguzo za maendeleao ulimwanguni ni viwanda. Viwanda ni muhimu kwa kuwa ndivyo vinavyoigeuza malighafi inayopatikana na kuwa bidhaa zinazoweza kutumiwa na watu. Katika nchi zinazoendelea, ambazo hazina uwezo mkubwa wa mitaji viwanda vinavyoimalika ni vile vidogo. Hivi ni viwanda ambavyo huhusiana na amali za mikono. Kuimatika kwa viwanda hivi kunatokana na sababu mbalimbali.

Nchi zinazoendelea huwa na masoko finyu sana kwa kuzingatia uwezo wa ununuzi wa wanaolengwa na bidhaa za viwanda. Katika msingi huu viwanda vitawiwa ugumu kufanya biashara katika mazingira ambako masoko yake ni finyu au utashi wa bidhaa zake sio mkubwa. Viwanda vodogo pia vinao uwezo wa kuwaajiri wafanyikazi wengi hasa kwa kuwa havina uwezo wa kugharamia mashine. Uajiri huu wa wafanyikazi wengi ni muhimu katika maeoneo mengi ambako tatizo la ajiri ni mojawapo wa hayana migumo imara ya kuwakimu watu wasiokuwa na kazi. Utegemezi wa jamaa wanaofanya kazi kwa hivyo unakuwa nyenzo ya pekee ya kuyamudu maisha.

Kuanzisha viwanda vidogo vidogo hakuhitaji mataji mkubwa tofauti na viwanda vikubwa. Hali hii inasahilisha uwezekano wa wartu wengi kujasurisha shughuli yoyote ile. Sambamba na suala j=hili ni kuwa ni rahisi kujarisha bidhaa mpya kwa kiwango kidogo cha kawaida. Ikiwa msahlishaji yeyote atazalisha bidhaa mpya kwa mapanu, kwa mfano kama ilivoyo kwa viwanda vikubwa, pana uwezekano wa kupata hasara kubwa. Huenda utashi wa bidhaa uwe mdogo ukilinganisha na ugavi wa bidhaa yenyewe. Majarinio mazuri ni kwa kiwango kidogo.

Kuwepo kwa viwanda vidogo huwa choche kubwa la usambazaji wa viwanda hadi maeneo ya mashambani. Hali hii inhakikisha kuwa nafasi za ajira zimezambazwa nchini hali ambayo inasaidia kuhakikisha kuwa pana mweneo wa kiununuzi wa umma. Huu ni msingi muhimu wa maendeleo. Aghalabu viwanda vikubwa huengemea kwenye mitaji ya mashirika ya kimataifa na huwa msingi wa kuenelezwa kwa utegemezi wa kiuchumi.

**Maswali**

(a) Kwa nini viwanda ni muhimu? (ala 2)

**Hugeuza malighafi inayopatikana kwa bidhaa za kutumiwa na watu.**

(b) Ni nini kiini cha matatizo au uuzaji wa bidhaa katika nchi zinazoendelea? (ala2)

**Masoko finyu kutokana na uwezo wa wanunuzi.**

(c) Eleza faida zinazotokana na kuwepo kwa viwanda vidogo (ala4)

**(i) Vina uwezo wa kuwaajiri wafanyakazi wengi**
**(ii) Hakuhitaji mtaji mkubwa**



Download this and other FREE materials from https://teacher.co.ke/notes

Teacher.co.ke

**(iii) Ni rahisi kujaribisha bidaa mpya kwa kiwango kidogo cha kiwanda kidogo.**
**(iv) Huwa chocheo kubwa la usambazaji wa viwanda hadi maeneo ya mashambani.**
**(v) Watu wengi wanaweza kuanzisha viwanda hivyo.**

(d) Usambazaji wa viwanda katika maeneo ya mashambani una faida gani? (ala 4)
**(i) Nafasi za ajira zimesambazwa.**
**(ii) Hutoa mweneo mzuri wa kimapatao**
**(iii) Huboresha uwezo wa kiununuzi wa umma**
**(iv) Ni msingi mkubwa wa kujitegemea kiuchumi.**

(e) Fafanua maana y msamiati huu kama ulivyotumika katika kifungu. (ala3)
**i) Kujasurisha - Kuanzisha**

**ii) Amali - Kazi**

**iii) Utashi Hamu**
- Adhibu kosa la kisarufi litokeapo mara ya kwanza hadi makosa sita (½ x 6 = 3)
- Adhibu Kosa la hijai litokeapo mara ya kwanza hadi makosa sita (½ x 6 = 3)
- Adhibu kosa la hijai hata pale amekosea jibu.

## MATUMIZI YA LUGHA (ALAMA 40)

1. Taja na ueleze aina mbili kuu za ala za matashi (ala 2)
**(i) Ala tuli – ala ambazo hazisogei sauti inapotamkwa.**
**(ii) Ala sogezi - ala ambazo husogea sauti inaptamkwa.**

Teacher.co.ke

2. Linganisha sauti zifuatazo (ala 2)
**(i) /dh/ na /th/ Zote ni sauti za menoni**

**(ii) /o/ na /u/ - zote mdomo huwa umeviringwa**

3. Onyesha silabi ambazo zitatiwa shadda katika maneno haya (ala 2)
**(i) Msisimko - m**

**(ii) Maswali - wa**

**(iii) Tafadhali - dha**

**(iv) Mchunga – chu**

4. Tunga sentensi ukitumia mofimu huru ambayo ni kivumishi (ala2)
**- Mtoto safi ametuzwa**
**- Mifano ya mofimu huru ambazo ni vivumishini hodari, jasiri, n.k.**

5. Ainisha viambishi katika kitenzi kifuatacho kidhamira (ala 3)
Aliyekufa
A – li – ye – ku – f - a

Download this and other FREE materials from https://teacher.co.ke/notes

Teacher.co.ke

**Nafsi/Ngeli wakati O rejeshi mtendwa mzizi kiishio**

6. Yakinisha katika wingi sentensi ifuatayo ( ala2)
   Wanafunzi walisoma vitabu hivyo
   **Wanafunzi walisoma vitabu hivyo**

7. Taja matumizi mawili ya paradesi (ala 2)
   **Hutumiwa kutoa maelezo zaidi**
   **Kutungia herufi au nambari**
   **Hutumiwa katikamaandishi ya kitamthilia ili kufungia mambo zaidi.**

8. Tunga sentensi ukitumia kiunganishi cha masharti (ala 1)
   **Baadhi ya viunganishi vya masharti ni kama vile; kama, ikiwa, iwapo, mradi.**

9. Tunga sentensi moja na uonyeshe aina mbili za vishanzi (ala 2)
   **Mzee aliyefika leo alikuwa mwema.**
   **Mzee alikuwa mwema – kishazi huru**
   **Aliyefika leo – kishazi tegemezi.**

Teacher.co.ke

10. Andika miundo mitatu ya ngeli ya U- ZI (ala 3)

   **(i) U – NY**
   **Uso – Nyuso**
   **Uma – Nyuma**
   **(ii) U – ND**
   **Ujiti – Njiti**
   **Ujukuti – Njukuti**

   **(iii) W – NY**
   **Waya – Nyaya**
   **Wakaa – Nyakaa**

11. Tunga sentensi yenye muundo ufuatao (ala 2)
   N+RH+t+E
   **Nguo ya mama ilishonwa vizuri**

12. Andika upya ukifuata maagizo (ala3)
(i) Maji ambayo wanakunywa ni hatari ( Andika katika hali ya mazoea bila kutumia "amba")
   **Maji wanywayo ni hatari.**

(ii) Watu wengi <u>walihasirika</u> bomo <u>lilipolipuka</u> katika jengo hilo (tumia nomino badala ya vitenzi vilivyo pigwa mstari)
   **Watu wengi walipata hasara kulipotokea mlipuko katika jengo hilo.**

13. Andika sentensi ifuatayo katika hali timilifu (ala 1)



Download this and other FREE materials from https://teacher.co.ke/notes

Teacher.co.ke

Waziri anasoma hotuba yake

**Waziri amekuwa akisoma hotuba yake.**

14. Tunga sentensi na uonyeshe kiima, kitondo na kipozi (ala3)

**Mama alimpikia mgeni nyama tamu**
**Mama – kiima**
**Mgeni – kitondo**
**Nyama tamu - Kipozi**

15. Changanua utungo ufuatao kwa muundo wa mstari ( ala 3)

Mimi nitaenda maktabani leo.

**S(KN + N + KT) KN (W) KT CT + E + E)**

16. Tunga sentensi kuonyesha majukumu matatu ya kiimbo. (ala3)

**Mtoto Analia.(sentensi ya taarifa)**
**Mtoto Analia!(sentensi ya kuonyesha mshangao)**
**Mtoto Analia?(sentensi ya kuonyesha swali)**

17. Andika sentensi ifuatayo katika kauli ya ketendewa (ala 2)

Nzi hawa wamemsumbua Musa kwa muda mrefu

**Musa amesumbuliwa na nzi hawa kwa muda mrefu.**

18. Taja methali inayoafiki maelezo yafuatayo (ala 1)

Mtu anayetegemea jamii akiondoka wanaomtegemea huwa mashakani

**Mti mkuu ukigwa wana wa ndege huyumba.**

19. Andika sentesi ifuatayo upya kwa kufuata maagizo kwenye mabano (ala 1)

Mama alimkaripia \]toto mtiro (anza kwa mtoto)

**Mtoto mtoro alikaripiwa na mama.**

## ISIMU JAMII (ALAMA 15)

20a) Eleza dhana ya isimu jamii ( ala 2)

**Tawi la isimu linalochunguza matumizi ya lugha katika jamii.**

b) Taja nadharia zozote tatu zinazoelezea chimbuko la Kiswahili (ala 3)



Download this and other FREE materials from https://teacher.co.ke/notes

Teacher.co.ke

**Kiswahili ni lugha ya kibantu**
**Kiswahili ni lugha mseto**
**Kiswahili ni lugha ya kiarabu.**

c) Eleza sifa zozote tano za sajili ya hospitalini ( 5)

**(i) Huwa kuna kutohoa kwa maneno kama vila bendeji, operesheni, daktari n.k.**
**(ii) Kuna matumizi ya istilahi maalumu kama vile VCT, CD4, tembe, machela.**
**(iii) Lugha ya mafumbo/Usiri k ama vile tumempoteza kwa maana ya amekufa.**
**(iv) Kuna matumizi ya lugha ya tarakimu kama vile 1 x 3**
**(v) Kuchanganya ndimi/msimbo, kwa mfano wawtoto w ote must be vaccinated.**
**(vi) Lugha ya kudadisi/Kuhoji kufahamu shida ya mgonjwa. k.g.**

**Daktari: Umeanza kuendesha lini?**
**Mgonjwa: Leo asubuhi**
**Daktari: Je, umekunywa dawa yeyote?**
**Mgonjwa: La**

**(Sharti mwanafunzi atolee mifano; bila mifano ondoa nusu).**

**USHAIRI ANDISHI: (ALAMA 5)**

21. Taja vipengele vyovyote vitano vinavyozingatiwa wakati wa kuainisha shairi kiumbo/muundo.

**(i) Mfangilio wa vina**
**(ii) Idadi ya mizani**
**(iii) Idadi ya vipande**
**(iv) Idadi ya beti**
**(v) Idadi ya mistari/ishororo katika ubeti. n.k.)**

Teacher.co.ke

## USHAIRI SIMULIZI

22. (a) Fafanua aina zifuatazo za nyimbo (ala 5)

**(i) Mbolezi - Nyimbo ambazo huimbwa wakati wa kuomboleza kama vile matanga, mazishi au janga.**

**(ii) Sifa/Tukuza – Huimbwa kumsifu mtu Fulani kwa mchango wakek katika jamii.**

**(iii)Wawe / Vave – Huimbwa wakati wa kulima.**

**(iv) Nyiso - Huimbwa wakati wa jando na unyago**

**(v) Bembea / Bembelezi - Huimbwa watoto kuwafariji au kuwabembeleza walale au waache kulia .**

(b) Eleza dhima ya nyimbo (ala 5)



Download this and other FREE materials from https://teacher.co.ke/notes

Teacher.co.ke

(i) **Nyimbo hutumiwa kama burudani, kufurahisha, kustarehesha na kusisimua.**
(ii) **Hukuza ubunifu mlangoni mwa wanajamii kwani uimbaji ni kipawa na nyimbo hupalilia kipawa hiki.**
(iii) **Hupitisha amali na mambo ambayo jamii inayathamini.**
(iv) **Ni mbinu mojawapo ya kuhifadhi na kuendeleza utamaduni wa jamii.**
(v) **Nyimbo husaidia binadamu kutakasa hisia zake.**
(vi) **Nyimbo hutambulisha jamii kwa kusawiri shughuli na maisha ya jamii ilizibuni.**

**(c) Fafanua sifa za wahusika wafuatao.(ala 15)**

**(i)Ridhaa**

**Ni mwenye bidii. Ni dakari ambaye alifanya kazi kwa uadilifu.**

**Ni msomi. Amesomea udaktari.**

**Mwenye uhusiano mwema. Anakula pamoja na majirani.**

**Ni mshirikina.anahusisha milio ya bundi na jambo mbaya kutokea.**

**Mwenye mapenzi. Anawapenda wanawe sana.**

**Ni mkarimu.anasaidia jamii kwa kujenga hospitali.**

**Amepevuka .anasema iwapo hakutakuwa na njia madhubuti ya kusuluhisha migogoro kunaweza shuka shida tena.**

**Ni mvumilivu.anavumilia kuona mabaki ya kuteketezwa kwa familia yake**

**(mwanafunzi lazima afafanue sifa zingine zozote.)**

**ii) Kaizari**

**Alikuwa babake mwanaheri na lime.**

**Ni mwenye busara.aliyajenga maisha ya familia yake upya baada ya kurejea kutoka msitu wa mamba**
**Ni mvumilivu. Alivumilia kuiona familia yake ikifanyiwa ukatili na vijana .**
**Ni msomi.amesomea utabibu.**
**Ni mwenye uhusiano mwema.anajihusisha na wakimbizi wengine kwenye msitu wa mamba.**
**Ni mwenye mapenzi .anawapenda wanawe na mke wake subira**

**(mwanafunzi afafanue sifa zingine zozote)**

**iii) Mwangeka**

**Ni mwanawe Ridhaa na Terry.**

**Ni msomi.ana shahada ya uhandisi.**



Download this and other FREE materials from https://teacher.co.ke/notes

Teacher.co.ke

**Ni mlezi mwema. Analea familia yake vizuri.**

**Ana uhusiano mwema.anajihusisha vizuri na familia yake.**

**Ni mzalendo.anaenda mashariki ya kati kuleta Amani.**

**Ni mkarimu.anaonyesha ukarimu kwa umu na nduguye Dickson.**

**Ana mapenzi ya dhati. Anampenda mke wake lily nyamvula.**

**Ana msimamo dhabiti.anaamua kujiunga na wanamaji hata baada ya rai ya mkewe lily.**

**(mwanafunzi afafanue sifa )**

Teacher.co.ke

Download this and other FREE materials from https://teacher.co.ke/notes